# WILAYA YA KIRINYAGA
# DARASA LA TANO MUHULA WA TATU
# KISWAHILI

PENPLUS KIRINYAGA

**Muda: Saa 1 dak 40**

***Chagua jibu lifaalo zaidi kujazia mapengo 1-15***

Mlango__1__ mwalimu __2__ Kiswahili __3___alikuwa wa __4___ kuingia katika darasa __5___ la tano. Kipindi __6___ asubuhi kilikuwa __7___ . Alitusabahi kama __8___ desturi __9___ . Baada ya shughuli ndogo ndogo za hapa na pale __10___ darasani, alianza kutuelezea __11___ kuandika hati safi__12___ darasani, __13___ pia maishani __14___ . Kisha alituita __15___ ubaoni tukaandika neno hati.

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| 1. | A. ulipofunguliwa | B.ulipofungwa | C. ulipofungulia | D. ulifunguliwa |
| 2. | A. ya | B.wa | C. cha | C. kwa |
| 3. | A.ndio | B. ndiyo | C. ndiye | D. ndivyo |
| 4. | A. kuanza | B. kwanza | C. kuwanza | D. kwenda |
| 5. | A.yetu | B. mwetu | C .kwetu | D. letu |
| 6. | A. kile cha | B. ile ya | C. hiyo ya | D. hii ya |
| 7. | A. yake | B. chake | C. lake | C.wake |
| 8. | A. iliyokuwa | B.lilivyokuwa | C. ilikuwa | D. ilivyokuwa |
| 9. | A. yetu | B. kwake | C. yake | D. wetu |
| 10. | A.ule | B. lile | C. zile | D. mle |
| 11. | A. jinsi ya | B. hali ya | C. vile ya | D. ukweli wa |
| 12. | A. siko tu | B. siyo tu | C. sio tu | D. sivyo tu |
| 13. | A. mbali | B. pale | C. bali | D. vile |
| 14. | A. yetu | B. mwetu | C. zetu | D. wetu |
| 15. | A. moja | B. mmoja | C. mojawapo | D. mmoja mmoja |

***Kutoka swali la 16-30 chagua jibu lililo sahihi***

16. Kamilisha sentensi

Choo hiki ni___ sana.

A. kisafi B. msafi

C. safi D.visafi

17. Herufi za a,e,i,o,u huitwa vokali au ___

A. irabu B. akrabu

C, akraba D. ibara

18. 'Sabalheri wanafunzi,' mwalimu Rosa aliwasalimia wanafunzi wake.Huo ulikuwa wakati wa ___

A. alasiri B. jioni

C. asubuhi D. adhuhuri

19. Akisami $^2/_3$ huitwaje?

A. Tusui tatu B. Thuluthi mbili

C. Tisa ya tatu D. Subui tatu

20. Kanusha : "Wewe umekuja"

A. Wewe haujakuja

B Wewe hujaja

C. Wewe haujaja

D.Wewe hujakuja

21. Upinde, chusa, teo na manati ni____

A. zana za kilimo

B. ala za muziki

C. vifaa vya seremala

D. zana za vita

22. Tumia kirejeshi 'amba' ipasavyo

Mkuki ___ ulitumiwa kumwua chui___alimla beberu ni huu.

A. ambao-ambao

B. ambao- ambazo

C. ambayo- ambaye

D. ambao- ambaye

23. Ni neno lipi halionyeshi adabu?

A. Asante

B. Tafadhali

C. Nipe

D. Niazime

24. Watu wakiwa wametengana na kuwa mbalimbali husemwa ni kama____

A. jua na mwezi

B. ardhi an mbingu

C. uta na upote

D. lila na fila

25. Tumia kiunganishi kifaacho .

Wavulana walikimbia ___mmoja tu.

A. ili

B. ila

C.wala

D.lakini

26. Utitiri, kereng'ende, kiroboto na mavu kwa jina moja ni___

A. wanyama B. nyuni

C. wadudu D. matunda

27. Ipi huwa si sehemu ya ndani ya mwili ?

A. Kongosho

B. Ini

C. Moyo

D. Kiwiko

28. Kamilisha kitendawili hiki

____ mbili zavuka mto.

A. Papa

B. Ng'ombe

C. Njia

D. Popo

29. Tunda 'lile' limeiva.Jina 'lile' ni___

A. kielezi

B. kiashiria

C. kiunganishi

D. kimilikishi

30. Nomino 'gazeti' hupatikana kwenye ngeli gani?

A. I - ZI B. U -YA

C. U - ZI D. LI -YA

***Soma hadithi hii kisha ujibu maswali 31-40***

Aisha ni ajuza , yaani mama mzee aliyekuwa na watoto wanane. Mume wake, Badi Jafari,alikuwa seremala aliyefanyia kazi zake za ufundi wa mbao kule Msambweni, mtaa wa vijana wenye bidii na vipawa vizuri. Ingawa baadhi yao hawakuwa wazuri katika masomo ya darasani , Mungu hakuwanyima talanta mbalimbali.

Aisha alibarikiwa kupata watoto watatu waliokuwa hodari wa kutunga na kuyaimba mashairi. Kati ya watoto hao watatu, Amal ndiye aliyejaliwa kuwa mwimbaji mzuri wa nyimbo za taarab.

Watoto wengine wanne walikuwa na ujuzi wa kufuma mikeka na kutengeneza vikapu. Watalii wengi walipenda na kutamani kukitembelea mara kwa mara kijiji cha Ramisi alikoishi Bwana Badi na jamaa yake.

Wanawe Aisha waliokuwa watunzi wazuri wa mashairi walipata njia za kujiendeleza baada ya watalii kuwanunulia vyombo vya kutumia wakati walipokuwa wakiwatumbuiza wageni mtaani Msambweni. Kijiji cha Ramisi kilipata sifa nyingi na kuwapa wengine imani ya kufanya bidii zaidi maishani. Kweli kwa Mungu, kila mtu ana siku yake.

31. Ni nani aliyekuwa fundi wa kutengeneza vitu vya mbao katika taarifa uliyoisoma?

A. Mala B. Aisha

C. Mungu D.Badi

32. Jamaa iliyozungumziwa katika hadithi hii hupatikana katika kijiji kipi?

A. Msambweni B. Ramisi

C. Mombasa D. Hatujaambiwa

33. Familia ya bwana Jafari ilikuwa na malenga wangapi?

A. 8 B. 3

C. 4 D. Wengi sana

34. Ni watoto wangapi waliokuwa na uwezo wa kuimba nyimbo za taarab na vile vile kutunga mashairi?

A. Mmoja tu B. Watatu

C. Wanne D. Wanane

35. Kulingana na hadithi hii, ni akina nani waliopata nafasi ya kujiendeleza haraka?

A. Watengenezaji wa vikapu

B. Watunzi wa mashairi

C. Maseremala

D.Waimbaji

36. Iwapo Aisha alikuwa ajuza, mume wake alikuwa ___

A. mbuyu B. buda

C . sahibu D. shaibu

37. Ni sahihi kusema kwamba ___

A. mtaa wa Msambweni ulikuwa na vijana wengi wenye vipawa vikubwa

B. jamaa ya Badi haikumcha Mungu

C. kila mtu Msambweni alikuwa mtunzi mwema wa mashairi

D. wanawe Aisha hawakuwa na bidii yoyote

38. Jamaa hii kwa jumla ina watu wangapi?

A. Wanane

B. Watano

C. Kumi

D. Hatujaambiwa

39. Kufaulu kwa familia ya Bw. Badi na Bi Aisha kunategemea____

A. bidii na uzembe wa watoto wao

B. maombi pekee kwa mwenyezi Mungu

C. bidii na matumizi mazuri ya vipawa vya watoto wao

D.bidii waliyonayo watoto wao shuleni

40. Hadithi hii inatupa funzo gani?

A. Mwimbaji ni bora kuliko mwandishi wa mashairi

B. Tuzae watoto wengi wenye vipawa vingi

C. Kila mtu lazima afaulu maishani hata kama ni maskini

D. Mungu humpa kila mtu kilicho chake na ni muhimu tuvitumie vipawa vyetu ipasavyo

***Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali 41-50***

Binti Imani Maliwaza alikuwa msichana mrembo aliyeishi katika nchi kavu iliyokaribiana na jangwa. Alikuwa hana chakula cha kutosha nyumbani.

Alikuwa mfugaji wa paka watatu, kasuku watano, mbwa sita, ng'ombe wawili na kobe watano. Alikuwa na mahindi kiasi kidogo sana katika ghala lake. Basi aliamua kuwapikia wanyama wake kitoweo cha ugali lakini alipoona kwamba hawajashiba, alikitoa chakula chake alichokitegemea na kuwapa wanyama . Huruma ilioje?

Hakika, maisha yake na wanyama yalikuwa kama chanda na pete.

Siku moja alipokuwa nyumbani na mifugo wake, aliusikia mngurumo wa kushtua kutoka nje ya mlango wa chumba chake.

"Ni mnyama yupi huyu anayenguruma nje?" Binti Imani alijiuliza. Alipofungua mlango alishangaa kumwona simbabuka mmoja mkubwa. Hapo tu, alianguka na kuzimia kwa sababu ya kuliona jinyama lile hatari ambalo lingeiangamiza mifugo wake.

41. Mbona Imani hakuwa na chakula cha kutosha nyumbani?
A. Kwa sababu ya ukavu wa nchi uliyokaribiana na jangwa
B. Alikuwa mfugaji wa wanyama wengi waliokimaliza chakula
C. Hakuwa mkulima shujaa na mahindi yalikuwa machache
D. Alikuwa mkulima wa mahindi pekee

42. Ni wanyama gani waliofugwa kwa wingi wa idadi?
A. Kasuku
B. Mbwa
C. Kobe
D. Paka

43. Alipogundua kuwa chakula hakitoshi, Imani aliamua kuwapikia wanyama chakula kipi?
A. Pure
B. Mchuzi
C. Kitoweo cha sima
D. Kitoweo cha kuku

44. Imani alipendana na wanyama wake kama ___
A. ushati na ngozi
B. usiku na giza
C. shilingi kwa aya pili
D. chanda na pete

45. Mngurumo uliomshtua Imani ulikuwa wa nini?
A.Gari
B. Simbabuka
C.Chui
D. Shetani

46. Simba alifanya nini baada ya Imani kuanguka na kuzimia?
A. Alimla Imani
B. Alikula mifugo wote
C. Alitoroka porini
D. Hatujaelezwa

47. Kutoa chakula ghalani na kuwapikia wanyama kunaonyesha kwamba Imani ni___
A. karimu
B. mchoyo
C. mkono birika
D. mpishi

48. "Alikuwa na mahindi kiasi kidogo." Maelezo haya yanamaanisha_____
A. mahindi hayakuwepo kabisa
B. hakuwa na mahindi yoyote katika ghala
C. mahindi yalikuwa haba
D. mahindi huliwa kidogokidogo na wanyama

49. Ghala pia huitwa_____
A bohari
B. zahanati
C. soko
D. ghorofa

50. Kichwa cha habari hii kinafaa kuwa___
A. Maliwaza mchoyo
B. Maliwaza mpenzi wa wanyama
C. Imani na simba
D. Umuhimu wa simba kwa wanyama